get ready QUEENSLAND

# Sikiliza Onyo!

Queensland Government

**Tunafurahia hali ya hewa na hali ya maisha nzuri hapa Queensland. Hata hivyo, majanga ya kimaumbile kama vile tufani, dhoruba, mafuriko na tsunami ni sehemu isiyoepukika katika mazingira yetu. Matukio ya hivi karibuni yameanza kutuonyesha kwamba hatuwezi kuchukulia mambo rahisi kuhusu hatari ambazo zinaletwa na majanga haya.**

Tafuta muda na utayarishe dharura kwa:

- Kutayarisha Mpango wako wa Dharura
- Kutayarisha Mkoba wako wa Dharura
- Kutayarisha nyumbani pako
- Sikiliza onyo

Huduma za Dharura hutumia mbinu anuwai katika kutoa onyo kwa jumuia kuhusu hali ya hewa kali na dharura nyinginezo ambazo zinahitaji matayarisho na hatua katika kiwango cha nyumbani. Wakati onyo zinatolewa unaweza kuelekezwa katika:

- Kukamilisha matayarisho
- Kusalimisha vitu vilivyo karibu na nyumbani
- Kuamilisha Mpango wa Dharura
- Kupata hifadhi mahali, au
- Kuanza kutolewa katika mahali palipoamuliwa mapema na ambapo ni salama zaidi

**Onyo ni za haraka** – utahitaji kuchukua hatua mara moja kuhusiana na taarifa iliyotolewa

## 1. Sikiliza:

- Sikiliza redio yako inayoendeshwa kwa betri kwenye kituo chako cha redio cha karibu zaidi cha ABC au kituo chako cha redio cha biashara kilicho karibu zaidi kwa habari za hali ya hewa na onyo.
- Tazama televisheni yako kwenye kituo cha televisheni kilicho karibu nawe ili utazame na usikilize kuhusu habari za onyo.

**Onyo ni za haraka - utahitajika kuchukua hatua mara moja kuhusu taarifa iliyotolewa.**
**Bila kujali ni dharura ipi, unahitajika kuweza...**
**Kusikiliza...Kuingia...Kutega sikio na Kuchukua hatua!**

## 2. Ingia:

- Katika tovuti ya Biuro ya Metorolojia kwa habari za hali ya hewa, onyo ya hali ya hewa na taarifa ya onyo kuhusu tsunami. www.bom.gov.au.
- Tovuti ya Huduma za Usimamizi za Janga za Queensland kwa taarifa kuhusu kutayarisha, Tahadhari ya Dharura iliyotolewa na taarifa ya sasa kuhusu matokeo ya Janga. www.disaster.qld.gov.au
- Tovuti yako ya karibu zaidi ya baraza kwa taarifa kuhusu mipango ya usimamizi ya dharura ya karibu nawe na mipangilio ikijumuisha taarifa ya kutolewa na njia za kutumika. www.dip.qld.gov.au/local-government-directory.html

## 3. Tega sikio:

- Kwa Ishara ya Onyo ya Dharura ya Wastani (SEWS) inayotumiwa mwanzo wa onyo kali.
- Kwa ujumbe wa sauti wa Tahadhari ya Dharura kupitia kwenye simu yako ya nyumbani na ujumbe wa simuni hadi kwenye simu yako ya mkononi.
- Kwa matangazo ya usalama wa jumuia iliyo karibu nawe (kwenye redio na televisheni) kwa ushauri na habari zaidi.
- Kwa ving'ora na matangazo ya sauti, kwamba Huduma za Dharura huenda zikatumika hali fulani.
- Kwa wafanyikazi wa Huduma za Dharura ambao wanaweza kubisha-mlango katika eneo lililo karibu nawe ili kupashana wakazi kuhusu onyo hizo.
- Kwa taarifa zaidi kuhusu Onyo za Hali ya hewa piga simu:

  Onyo za Tropical Cyclone QLD:
  1300 659 212

  Onyo za Hali ya hewa ya Ardhini na ya Mafuriko QLD: 1300 659 219

  Onyo za QLD Baharini ya Pwani:
  1300 360 427

  Taarifa kuhusu Tishio la Tsunami ya Australia:
  (1300 TSUNAMI)
  1300 878 6264
  Onyo za Kawaida za QLD
  1900 969 922 (gharama za kupiga simu zinatumika)



## 4. na Chukua hatua:

- Chukua hatua mara moja kuhusu ushauri uliyotolewa
- Hakikisha wanafamilia wote wanajua onyo na ushauri uliyotolewa. Angalia jirani na rafiki ambao huenda wakahitaji msaada maalum
- Amilisha Mpango wako wa Dharura wa Familia
- Tafuta na uchukuwe Mkoba wako wa Dharura
- Amilisha mipangilio yako yote ya kutolewa kama itahitajika.

Kama unatembelea ama uko likozo katika Queensland au jimbo lingine na huna familia au urafiki wa kupata hifadhi, wasiliana na msimamizi wako wa malazi ili atambue machaguo yaliyopo ya kutolewa.

**EMERGENCY ALERT.**
**BE WARNED. BE INFORMED.**

Tahadhari ya Dharura ni mfumo wa onyo kupitia kwenye simu ambao mamlaka wanaweza kutumia ili kutoa onyo kwa jumuia.

Tahadhari ya Dharura inaweza kutumiwa katika tadadhari za sauti kupitia kwa simu za nyumbani kulingana na mahali pa kupokea simu, na tahadhari za ujumbe kupitia kwenye simu za mkononi kupitia kwenye anwani ya kulipia.

Ni kwa matumizi ya hali anuwai za dharura zikiwemo matokeo kali ya hewa na moto za msitu. Hutatozwa na hautalazimika kulipia kwa onyo ya tahadhari yoyote. Muhimu zaidi, huwezi kutoka kwenye huduma hiyo ya kupokea tahadhari za dharura.

Kama utapokea Tahadhari ya Dharura, unahitaji kuisikiliza kwa makini katika shauri huo uliotolewa na huchukua hatua mara moja. Ujumbe wa sauti utarudiwa endapo utashikilia laini. Huenda ukaelekezwa kumaliza matayarisho, kusalimisha vitu karibu na nyumbani pako, kupata hifadhipale mahali au kuanza kutolewa hadi mahali penu palipoamuliwa palipo salama zaidi. Kwa taarifa zaidi nenda katika: www.disaster.qld.gov.au/ea/emergencyalert.asp

**stop&listen**
Standard Emergency Warning Signal

Wakati onyo zinapotolewa kwa dharura kuu, mamlaka yanayofaa huenda yakatumia Ishara ya Onyo ya Dharura Wastani (SEWS) kabla ya kutoa taarifa kuhusu dharura hiyo.

SEWS ni king'ora kinachopiga kilele kinachotumiwa kote Australia kwa matukio ya dharura muhimu kama vile tufani, moto wa msitu, mafuriko na dhoruba kali. Wakati unaposikia ishara kwa redio, televisheni au kupita kwenye simu kwa ujumbe wa Tahadhari ya Dharura, tilia maanani taarifa itakayofuata na uchukue hatua mara moja kuhusiana na ushauri huo uliotolewa.

Ili kusikiliza SEWS nenda katika:

www.disaster.qld.gov.au/disasters/warning.asp



# Sikiliza Onyo!

**SIKILIZA, INGIA,TEGEA SIKIO NA CHUKUA HATUA**

**Sikiliza:**

Kituo changu cha Radio kilichokaribu nami:

Kituo changu cha televisheni kilicho karibu nami:
:___________________________

**Ingia:**

Biuro ya Metorolojia (BoM) www.bom.gov.au
Biuro- Ukurasa Wangu uliokaribu nami:

___________________________
Huduma za Usimamizi wa Majanga Queensland

www.disaster.qld.gov.au

Tovuti yangu ya Baraza lililokaribu nami:

___________________________

**Sikiliza:**

www.disaster.qld.gov.au/disasters/warning.asp
www.disaster.qld.gov.au/EA/Emergencyalert.asp

Biuro - Nambari Yangu Iliyokaribu Nami:

___________________________
Taarifa ya Tsunami
1300 TSUNAMI (1300 878 6264)

**Chukua Hatua:**

Onyo ni za dharura
Chukua hatua mara moja katika taarifa iliyotolewa.

Kwa taarifa zaidi
kujitayarishia dharura tembelea:

www.disaster.qld.gov.au

## Taarifa ya Mawasiliano ya Dharura

| | | |
|---|---|---|
| Polisi – Moto - Ambulensi | Sufuri Mara Tatu (000) (112 kutoka kwenye simu ya mkononi) | www.safer.qld.gov.au/Emergencies/Triple_Zero |
| Biuro ya Metorolojia | | |
| Onyo za Kawaida za QLD | 1900 969 922 (gharama za kupiga simu zinatumika) | www.bom.gov.au |
| Onyo za Tufani ya Tropical ya QLD | 1300 659 212 | www.bom.gov.au/cyclone |
| 1300 659 212 | 1300 659 219 | www.bom.gov.au/hydro/flood/qld |
| Onyo ya Baharini ya Pwani ya QLD | 1300 360 427 | www.bom.gov.au/marine |
| Taarifa ya Tishio ya Tsunami Australia | 1300 TSUNAMI 1300 878 6264 | www.bom.gov.au/tsunami |
| Ishara ya Onyo ya Dharura ya Wastani (SEWS) | | www.disaster.qld.gov.au/disasters/warning.asp |
| Kitabu cha Orodha cha Serikali iliyo karibu nawe. | | www.dip.qld.gov.au/local-government-directory.html |
| Afya na Hospitali | 13 HEALTH (13 43 25 84) | 13 HEALTH (13 43 25 84) |
| Shule | | www.education.qld.gov.au |
| Utoaji wa umeme/Kupotea kwa umeme -Nyaya za umeme zilizoanguka South East QLD: | Energex: 13 19 62 | www.energex.com.au |
| QLD nyingine zote. | Ergon Energy: 13 16 70 | www.ergon.com.au |
| -Ugavi na kupotea South East QLD: | Energex: 13 62 62 | |
| QLD nyingine zote. | Ergon Energy: 13 22 96 | |
| Kufungwa kwa Barabara - QLD Kusini Mashariki: | 13 19 40 | www.131940.qld.gov.au |
| QLD nyingine zote. | 1300 130 595 | |
| Simu Telstra: | 132 203 | www.telstra.com.au |
| Optus: | 1300 307 937 | www.optus.com.au |
| Wanyama LainiHaraka ya Wanyama wa Porini | 1300 130 372 | |
| RSPCA | 1300 852 188 | www.rspcaqld.org.au/emergencies |
| Nambari ya simu ya Uangalizi wa Ugonjwa (repoti Magonjwa ya Wanyama) | 1800 675 888 | www.dpi.qld.gov.au/27_127.htm |
| Wanyama waliopotea/wasioonekana | | http://lostfound.rspcaqld.org.au/ |

Broshua hii ni ya taarifa pekee na imetolewa kwa roho safi. Idara ya Usalama wa Jumuia, Usimamizi wa Dharura wa Queensland na Huduma ya Dharura ya Serikali yote haitawajibikia mtu yeyote kwa mujibu wa kupoteza au kuharibika kokote (kukiwemo athari ya kupoteza au kuharibu) ambayo kunaweza kupatikana au kutozwa, au kunakoweza kutokea moja kwa moja au vinginevyo, kwa mujibu wa kutegemea wa mtu yeyote katika taarifa ilimo kwenye broshua hii.

Queensland Government